

MAJUKWAA YA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI

Serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kwa kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji na Uendeshaji Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi. Mwongozo huu ulizinduliwa tarehe 12 Septemba, 2022, na unalenga kuimarisha na kuboresha uanzishaji, uendeshaji, usimamizi, uratibu, na muundo wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika ngazi ya Taifa, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Serikali imeandaa Mwongozo ambao ni msingi wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa majukumu ya majukwaa haya, na hivyo kuchochea mafanikio ya shughuli za kiuchumi na kijamii zinazohusisha wanawake katika maeneo mbalimbali

Malengo mahsusini ya mwongozo huu ni:

- Kuweka utaratibu wa kuunda, kuendesa, na kuboresha Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- Kuelekeza utaratibu au hatua za uanzishwaji wa Majukwaa;
- Kuainisha utaratibu au hatua za uanzishwaji wa Jukwaa;
- Kuainisha majukumu ya wasimamizi wa jukwaa katika kila ngazi;
- Kufafanua mfumo au muundo wa utekelezaji wa majukumu ya kila mdau katika utekelezaji wa Jukwaa.

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKWAA YA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2023/2024, majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi yalionesha ongezeko kubwa katika maeneo mbalimbali. Kwa upande wa wanachama, idadi iliongezeka kutoka **14,110** mwaka 2022/2023 hadi **626,822** mwaka 2023/2024, ikiwa ni ongezeko kubwa la **612,712** wanachama. Hii inaonesha mafanikio ya utekelezaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, ambapo zaidi ya **asilimia 4000** ya wanachama waliongezeka mwaka mmoja tu. Hivyo, Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi yameonesha ongezeko kubwa kutoka mwaka 2022/2024 hadi 2023/2024 katika maeneo mbalimbali, kama vile ngazi za Halmashauri, Kata, Vijiji, na vitongoji. Ongezeko hili

linaashiria juhudini za kuongeza ushiriki wa wanawake katika shughuli za kiuchumi na kuongeza idadi ya wanachama wa majukwaa katika Mikoa mbalimbali. Takwimu za majukwaa pia zimechambuliwa na kuainishwa kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 01 hapa chini linaonesha mafanikio ya utekelezaji wa mikakati ya Serikali ya kuhamasisha wanawake kushiriki katika shughuli za kiuchumi, ikiwa ni pamoja na upanuzi wa majukwaa, ongezeko la wanachama, na juhudini za kuhakikisha ushiriki wa wanawake katika shughuli za biashara, kilimo, na sekta nyingine za kiuchumi.

Jedwali Na. 01: Mwenendo wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mwaka	Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi						
	Halmashauri	Kata	Vijiji	Mitaa	Vitongoji	Majukwaa Kimko	Jumla ya Wanachama
2023/2024	161	2,721	8,240	868	5,620	17,670	626,822
2022/2023	26	151	33	1,354	2,885	1,859	14,110